

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO  
(BaruazoteziandikwekwaMkurugenziMtendaji [W])

SimuyaMdomo:  
023 - 2440164  
Fax: 023 - 2440338



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W),  
S. L. P. 59,  
BAGAMOYO.  
MKOA WA PWANI.

Kumb.Na. HWB/E.50/26/VOL.II/48

Tarehe: 09/09/2019

## TANGAZO NAFASI YA KAZI

### NAFASI KAZI:

1. WAANDIKISHAJI WAPIGA KURA 167
2. WAANDIKISHAJI WA AKIBA 167

Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) sura ya 287 na Kanuni za Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2019, anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa tumeanza maandalizi ya Uchaguzi wa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji na Vitongoji unaotaarajiwa kufanyika tarehe 24 Novemba 2019.

Ili kufikia azma hiyo tutaanza na zoezi la Uandikishaji wa Wapiga kura ambalo linatarajiwa kufanyika tarehe **8- 14 Oktoba 2019** na litafanyika kwa muda wa siku 7

Ili kufanikisha hilo tunahitaji watumishi wa Umma watakaofanya kazi ya kuandikisha Wapiga kura katika vituo 167 vya kupigia kura (kila kitongoji ni kituo cha kujiandikisha)

### **SIFA ZA MWOMBAJI NI KAMA IFUATAVYO;**

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Awe mkazi wa Bagamoyo
3. Asiwe na dhamana au kiongozi katika chama chochote cha siasa
4. Awe mwadilifu.
5. Mtunza siri

6. Awe tayari kufanyakazi husika kwa maelekezo yote
7. Awe amemaliza elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea.
8. Awe na umri wa miaka 18 – 60.
9. Awe ni mtumishi katika utumishi wa Umma (Public Servant). Aidha ainisha na Check Namba, kazi unayofanya na kituo cha kazi na namba ya simu.
10. Watendaji wa Kata na Vijiji hawaruhusiwi kuomba kazi hii.

Mwombaji awe tayari kulipwa **Tshs 20,000/=** kwa siku na kazi hii itadumu kwa muda wa siku 7.


Maombi yaandikwe kwa maandishi ya kalamu (yasichapishwe) na kupitishwa na Afisa Mtendaji Kata, hakikisha umejiorodhesha kwenye orodha ya waombaji katika kata husika ya watumishi. Maombi yatumwe kwa anuani:-

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 59,  
BAGAMOYO**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **17/09/2019** saa **9:30** jioni katika Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata yako atakayewasilisha ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.

**TANGAZO HILI PIA LINAPATIKANA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI**  
**[www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 10/09/2019.**

  
Fatuma O. Latu  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
BAGAMOYO**

**Nakala:** Watendaji wa Kata na Vijiji Wote  
Halmashauri ya Wilaya,  
**BAGAMOYO**

Mbao zote za Matangazo  
Halmashauri ya Wilaya  
**BAGAMOYO**